# HALMASHAURI YA MJI NJOMBE



halmashauri ya mji njombe www.njombetc.go.tz



TULIPOTOKA



TULIPO SASA

# SOKO KUU NJOMBE

# TAHARIRI



Salaam Ndugu Msomaji,


Karibu katika toleo rasmi la Jarida letu la Halmashauri ya Mji Njombe. Jarida hili linabeba dhana nzima ya kazi zinazotekelezwa na matukio mbalimbali yanayofanyika katika Halmashauri. Aidha toleo hili linajumuisha taarifa za kazi zilizofanyika katika robo ya kwanza na ya pili ya Mwaka 2020/2021.

Halmashauri ya Mji Njombe tumeuanza Mwaka 2021 tukiwa na ari mpya ya kuendeleza mapambano ya maendeleo kwa kuendelea kufikisha huduma karibu na Wananchi waliopo katika Halmashauri yetu.

Mwaka Jana tulifanya vizuri katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Mwaka huu tutafanya vizuri zaidi.Tuendelee kukusanya mapato kwa kasi ya juu. Mapato ndio muhimili mkuu wa mafanikio tuliyoyafikia na tunayotarajia kuyafikia.

Furahia kulisoma jarida letu kwa undani ili uweze kufahamu zaidi kuhusu Halmashauri yetu.

I. L. Mwenda,
Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji Njombe





*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Selemani Jafo akipata maelekezo ya Majengo yanayojengwa katika Kituo cha Afya Kifanya kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe Illuminatha Mwenda wakati wa Ziara yake Katika Halmashauri hiyo.*

# Ujenzi wa Vituo vya Afya Kifanya na Makowo Wamfurahisha Jafo. Ahaidi Vifaa Tiba Kifanya

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Selemani Jafo amefurahishwa na ujenzi wa Vituo vya Afya Kifanya na Makowo ambapo asilimia kubwa ya ujenzi wa vituo hivyo unatekelezwa kutokana na makusanyo ya mapato ya ndani na nguvu za Wananchi ambapo zaidi ya Shilingi milioni mia saba za mapato ya ndani zimepelekwa kwenye vituo hivyo.

Akizungumza Mara baada ya kukagua shughuli za Ujenzi Katika Kituo cha Afya Kifanya ambapo Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikipatia kituo hicho kiasi cha Shilingi Milioni kumi kusaidia ujenzi, Waziri Jafo amesema kuwa jitihada zilizofanyika kupitia makusanyo ya mapato ya ndani kwa kujenga vituo vya afya viwili ni kubwa na amezitaka Halmashauri nyingine kuiga Mfano huo.

“Kituo ni kizuri na Kimejengwa kwa mapato ya ndani.Tunavyozungumza juu ya vituo vya afya 487 sasa tunakwenda mpaka vituo mia tano. Ninyi Mko vizuri. Niwapongeze kwa kazi kubwa mliyofanya Mimi nimeona kuwa mnafanya kazi nzuri endeleeni na kasi hii. Majengo haya yanakwenda kuwahudumia Wananchi .Hata ukienda kukusanya ushuru Mwananchi anakuelewa. Sio unakwenda kukusanya ushuru lakini matokeo yake hayaonekani.Naomba niwapongeze. Mnyonge Mnyongeni lakini Haki yake mpeni”Alisema Waziri Jafo.

Jafo anaendelea kusema licha ya kuwepo na kasi ya ujenzi Vituo vya Afya Serikali pia imeendelea kutoa ajira kwa Wataalamu wa Sekta hiyo ili kuhakikisha kuwa vituo hivyo vinafanya kazi na kutoa huduma iliyo bora ambapo zaidi ya Wataalamu wa Afya elfu kumi na mbili (12,000)waliweza kuajiriwa katika kipindi hiki kwa awamu tofauti. Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini Deo Mwanyika na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe Illuminatha Mwenda wamemshukuru Waziri Jafo kwa kuweza kukagua ujenzi wa kituo hicho ambapo katika ziara hiyo ameweza kufanya mawasiliano na Katibu Mkuu TAMISEMI ili kuweza kupata vifaa katika kituo hicho.

"Mheshimiwa Rais alituchangia milioni 10, Wananchi Wamechangia milioni 28 Halmashauri ya Mji Njombe imechangia milioni 370 ambapo sasa tupo katika hatua za mwisho za umaliziaji. Makadirio yetu ni milioni 420 kukamilisha ujenzi ambao utakuwa msaada mkubwa kwa Wakazi wa ene la Kifanya na maeneo ya jirani."Alisema Mwenda.

Naye Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini Deo Mwanyika anasema"Mheshimiwa Jafo ametutia moyo sana nilimweleza juu ya uwepo wa vituo vya Afya viwili Kifanya na Makowo.Tumemwomba Vifaa. wakati wa Kampeni niliwaambia Wananchi Serikali imejenga kituo cha Afya na tutahakikisha kuwa kinapata vifaa na Wataalamu wakutosha na tumepata majibu ya vifaa. Tunashukuru sana.Wananchi wa Kifanya watambue sasa Serikali yao ipo kazini."

Awali katika ziara hiyo Mheshimiwa Jafo alipata nafasi ya kuzungumza na Watumishi kutoka katika Halmashauri ya Mji Njombe ambapo amesisitiza suala la ukusanyaji mapato na kufanya matumizi sahihi na amewataka wakurugenzi wote Nchini kuhakikisha kuwa ifikapo Mwishoni mwa mwezi Desemba Halmashauri zote 185 ziwe zimekusanya zaidi ya asilimia 50 ya lengo ambapo tarehe 15 Januari atatoa taarifa ya ukusanyaji mapato kwa kila Halmashauri kwa kipindi cha miezi sita. Pia amewataka Wakurugenzi kuhakikisha kuwa fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya elimu madarasa na mabweni ifikapo tarehe 30 Desemba miradi iwe imekamilika.




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI akizungumza na Watumishi wa Halmashauri ya Mji Njombe (hawapo pichani) wakati wa ziara yake katika Halmashauri hiyo.*

# Halmashauri ya Mji Njombe yatoa milioni mia saba laki tisa kwa vikundi 72

Halmashauri ya Mji Njombe imetoa kiasi cha Shilingi milioni mia saba laki tisa kwa vikundi 72 vya kiuchumi vya Wanawake, Vijana na Walemavu kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2020/2021.
Kiasi hicho cha fedha kinatokana na makusanyo ya mapato ya ndani ambapo kiasi cha Shilingi milioni 120 zimechangiwa, huku kiasi kilichosalia ikiwi ni fedha za marejesho.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi mfano wa hundi kwa vikundi hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhandisi Marwa Rubirya amevitaka vikundi hivyo kufanya matumizi sahihi ya mikopo hiyo ili kuwa endelevu na kufanya marejesho kwa wakati jambo litakaloviwezesha vikundi vingine kukopa.




*Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhandisi Marwa  Rubirya akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Shilingi Milioni mia saba laki tisa ikiwa ni asilimia kumi ya mapato ya Halmashauri kwa wawakilishi wa vikundi vya Wanawake,Vijana na Walemavu hafla iliyofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji Njombe*

“Mikopo hii ikatumike kwa malengo yaliyokusudiwa. Sio mnatumia fedha hizi kama kikundi mkifika kule mnagawana.Mwingine anaenda kununua baiskeli mwingine anaenda kulipa ada ya shule. Hayo sio malengo ya mkopo huu.”

Awali akiwasilisha taarifa ya hali ya utoaji wa mikopo katika Halmashauri Afisa Maendeleo ya Jamii Enembora Lema amesema kuwa Hali ya utoaji wa mikopo katika Halmashauri imeendelea kuimarika kila wakati kwani kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ilitoa TSH. 375,733,00, Mwaka 2019/2020 ilitoa TSH. 676,300,000 na Mwaka 2020/2021 kwa robo ya kwanza pekee Halmashauri imeanza kwa kutoa TSH  700,900,000/=

Kwa upande wao mwakilishi kutoka kundi la walemavu na wanawake wamesema kuwa ni vyema wanavikundi kutumia fedha hizo kuchochea shughuli za maendeleo jambo litakalopelekea kufanya marejesho kwa wakati.

“Tukisema tuchepushe kidogo hii fedha marejesho yatatushinda.Tutaanza kulalamika fedha ya Halmashauri inamkosi kumbe mkosi ni sisi wenyewe.”Alisema Mwakilishi wa Wanawake.

Aggrey Chatanda ni Mwakilishi kutoka Kundi la vijana amesema kuwa fedha hizo zitakwenda kuongezea nguvu kwenye mradi wa nyuki ambao tayari umeanza.

Utaratibu wa Utoaji wa mikopo bila riba kwa vikundi vya Wanawake,Vijana na Wenye ulemavu ulianzishwa ili wanufaika waweze kupata mitaji na kufanya uwekezaji katika shughuli za kiuchumi, Mathalani katika Kilimo,Ufugaji,Uvuvi na kuanzisha viwanda vidogo vidogo na hatimaye kuweza kuboresha Maisha kuanzia ngazi ya Familia,Jamii na Taifa.



*Sehemu ya Wanavikundi walioshiriki katika hafla ya makabidhiano ya hundi ya mfano wakiwa katika ukumbi wa Halmashauri*

# Milioni kumi za mapato ya ndani zatumika kununua taulo za Kike kwa Shule za Sekondari




*Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi. Ruth Msafiri akikabidhi Boksi zenye taulo za kike kwa Mmojawapo wa Wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Mpechi makabidhiano yaliyofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri Lunyanywi.*

Halmashauri ya Mji Njombe imeweza kutekeleza kikamilifu agizo la Serikali kwa kuzitaka Halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa taulo za kike ambapo kiasi cha shilingi milioni kumi kiliweza kutumika kwa ajili ya ununuzi wa taulo hizo kwa Shule za Sekondari.

“Kwa kuanza Halmashauri imeweza kutenga kiasi cha Shilingi milioni kumi ambapo Halmashauri imeweza kununua maboksi 260 ambapo kila boksi lina paketi 24 na kufanya jumla ya taulo sitini na mbili elfu na mia nne ambazo zitagawiwa kwa Shule zote 24 zenye wanafunzi wa kike katika Halmashauri ya Mji Njombe.” Alisema mratibu wa mpango ngazi ya Halmashauri Joyce Ngata.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano kwa wanafunzi wa kike Mkuu wa Wilaya ya Njombe Bi Ruth Msafiri amesema kuwa kwa sasa taulo za kike limekuwa si jambo la aibu kama ilivyokuwa zamani na imekuwa ni sehemu ya usafi kwa mtoto wa kike na ameipongeza Halmashauri kwa kutekeleza maagizo hayo.

“Serikali pia imeweza kuliwekea mkazo na Halmashauri imeweza kulitekeleza kwa kasi kubwa. Hii ikawe ni utunzaji bora wa afya za  wanafunzi wa kike  waelekezwe namna nzuri ya uhifadhi mara baada ya matumizi ili zisisababishe uchafuzi wa mazingira.” Alisema Mkuu wa Wilaya

Aliendelea kusema “Tuwasaidie watoto wakike wasiweze kupoteza masomo. Kuna kipindi watoto wa kike wana-shindwa kwenda shuleni kwa kukosa hifadhi nzuri.

Kwa upande wake Mkuu wa  Shule ya Sekondari Mbeyela Valeno Kitalika amesema kuwa Taulo hizo zitakuwa msaada mkubwa kwa Wanafunzi wa kike kwani kuna wazazi wanoshindwa kumudu gharama za kununua vifaa hivyo kupelekea watoto wa kike  kushindwa kuhudhuria shuleni katika kipindi wawapo katika mizunguko yao.

Wakipokea taulo hizo baadhi ya wanafunzi kutoka shule ya Sekondari Agness Trust Tumaini Maheve na Sayuni Festo Mhagama kutoka Shule ya Sekondari Maheve wamesema kuwa taulo hizo zitawasaidia kuweza kuhudhuria vipindi vyote vya darasani  na kuwafanya kuwa huru zaidi.

Halmashauri inaendelea na utaratibu wa kutenga fedha na kuhakikisha kuwa katika kila mwaka taulo za kike zinanunuliwa kwa wanafunzi kuanzia ngazi ya Msingi mpaka Sekondari.




*Wawakilishi  wa  Wanafunzi wa kike kutoka Shule za Sekondari za Halmashauri ya Mji Njombe walioshiriki katika zoezi la utoaji wa taulo za kike.*

# “Boda kwa Boda” Vita dhidi ya udumavu Njombe




*Meneja wa Mradi Tubadilishe Khadija Khalid akikabidhi pikipiki 4 kwa Mweka Hazina wa Halmashauri Dorcas Mkello ambaye pia alimwakilisha Mkurugenzi wa Halmashauri ikiwa ni jitihada za wadau kuwezesha usimamizi wa shughuli za lishe kwenye Halmashauri.Kushoto ni Afisa Lishe wa Halmashauri Marselina Mtitu na Oddo Msemwa wakifuatiwa na Afisa Usafirishaji wa Halmashauri Joshua Ngilangwa na Msimamizi wa Ofisi Emmanuel Kisela.*

Halmashauri ya Mji Njombe imeendelea na Mapambano dhidi ya udumavu ambapo imepokea Pikipiki 4 kutoka kwa mradi wa TUBADILISHE zitakazosaidia kwenye mapambano hayo.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya Pikipiki hizo kwa Halmashauri Meneja wa Mradi Tubadilishe inayohudumu katika Mikoa ya Njombe na Iringa Khadija Khalid amesema kuwa Pikipiki hizo zitatumika kusimamia shughuli za lishe katika Kata 08 zenye mradi Lengo ikiwa ni kurahisisha usafiri kwa Maafisa Ugani. Usafiri wa Pikipiki ni nafuu. Mafuta,matengenezo na zinafika kila sehemu hivyo itarahisisha kufikia kaya nyingi zaidi na kwa muda mfupi.” Alisema Khadija

Kwa upande wake Afisa Lishe wa Halmashauri Marselina Mtitu amesema kuwa pikipiki hizo ni msaada mkubwa katika Halmashauri ya Mji Njombe ambayo kwa sasa kwa mujibu wa takwimu Halmashauri inaongoza kwa kuwa na asilimia 53.6 za udumavu Kitaifa.Akipokea kadi na pikipiki hizo kwa niaba ya Mkurugernzi Mweka hazina wa Halmashauri Dorcas Mkello ameshukuru Mradi wa Tubadilshe kwa msaada huo na amewaomba wadau kuendelea kusaidia katika kuelimisha Wananchi na kuhamasisha jamii kuwa na lishe bora.

Halmashauri ya Mji Njombe inaendelea kufanya jitihada kuhakikisha kuwa udamavu unatokomezwa na jamii inakuwa na afya bora.

# Fahamu Baraza Jipya la Waheshimiwa Madiwani Halmashauri ya Mji Njombe

Halmashauri ya Mji Njombe imepata Baraza Jipya la Waheshimiwa Madiwani mara baada ya kula kiapo na kufanya uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu wake ambapo Mhe Romanus Clemence Mayemba Diwani wa Kata ya Njombe Mjini alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri na Mhe, Erasto Bernad Mpete (Diwani wa Kata ya Utalingolo kuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri.

Akizungumza mbele ya waheshimiwa Madiwani, Wataalam, waandishi wa habari na wananchi waliohudhuria tukio hilo Mhe. Hakimu aliyeongoza viapo hivyo amesema "Nawapongeza kwa kupata ushindi kwenye kata zenu nendeni sasa mkawatumikie wananchi ili kuleta maendeleo katika maeneo yenu". Aidha nawasisitiza mkawe mstari wa mbele katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Aliongeza Hakimu.



*Picha ya pamoja ya Baraza la Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Mji Njombe mara baada ya kuapishwa na kufanya uteuzi wa Kamati za Kudumu. 2020-2025*

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Wilaya ya Njombe George Emmanuel amesema ili kufuata misingi ya utawala bora ni vyema kuhakikisha kuwa Madiwani wanashiriki katika kuwaletea Wananchi Maendeleo na sio kuwa kikwazo cha kufanikisha maendeleo. Aidha Katibu Tawala amewataka Waheshimiwa Madiwani kufanya kazi kwa pamoja kujituma na kushirikiana na amewapongeza Waheshimiwa Madiwani wote kwa kuchaguliwa na kuwashukuru Wananchi wote na Viongozi wa Dini kwa kuliombea Taifa.

# ORODHA YA BARAZA JIPYA LA WAHESHIMIWA MADIWANI- HALMASHAURI YA MJI NJOMBE



MHE. ROMANUS CLEMENCE MAYEMBA
DIWANI WA KATA YA NJOMBE MJINI
MWENYEKITI WA HALMASHAURI
NAMBA YA SIMU 0767366738



MHE. ERASTO BERNAD MPETE
DIWANI WA KATA YA UTALINGOLO
MAKAMU MWENYEKITI WA HALMASHAURI
NAMBA YA SIMU 076735504



MHE. DEODATUS PHILIP MWANYIKA
MBUNGE NJOMBE MJINI
0747555999



MHE. EDWIN MWALONGO MWANZINGA
DIWANI KATA YA MATOLA
NAMBA YA SIMU 0768713399



MHE. FILOTEUS ANTON MLIGO
DIWANI KATA YA LUGENGE
NAMBA YA SIMU 0768100416



MHE. JACTAN NICHOLAUS MTEWELE
DIWANI KATA YA UWEMBA
NAMBA YA SIMU 0714047580



MHE. ALFRED JOHN MSIGWA
DIWANI KATA YA IHANGA
NAMBA YA SIMU 0767577336



MHE. ULRICK SIXTUS MSEMWA
DIWANI KATA YA LUPONDE
NAMBA YA SIMU 0765802753




MHE. NOLASCO BENEDICT MTEWELE
DIWANI KATA YA KIFANYA
NAMBA YA SIMU 0767438129




MHE. HONOLATUS PILIMINI MGAYA
DIWANI KATA YA MAKOWO
NAMBA YA SIMU 0755777950



MHE. GEOFREY BERNAD MHANDO
DIWANI KATA YA IWUNGILO
NAMBA YA SIMU 0625306860



MHE. NESTORY FEDRICK MAHENGE
DIWANI KATA YA MJIMWEMA
NAMBA YA SIMU 0755373880



MHE. NICKSON NICHOLAUS NGANYANGE
DIWANI KATA YA RAMADHAN
NAMBA YA SIMU 0754498360



MHE. MICHAEL MATHIAS UHAHULA
DIWANI KATA YA YAKOBI
NAMBA YA SIMU 0766311616



MHE. ANGELA CHARLES MWANGENI
DIWANI VITI MAALUM NJOMBE MJINI
NAMBA YA SIMU 0767490545



MHE. COLLETA PANKRAS NYIGU
DIWANI VITI MAALUM IGOMINYI
NAMBA YA SIMU 0769760990



MHE. TUMAINI JACKSON MTEWA
DIWANI VITI MAALUM NJOMBE MJINI
NAMBA YA SIMU 0756899621



MHE. MARIAMU SHABANI CHUNDU
DIWANI VITI MAALUM IGOMINYI
NAMBA YA SIMU 0763239253



MHE. CATHERINE SIMONI MWALUFUNA
DIWANI VITI MAALUM IGOMINYI
NAMBA YA SIMU 0759184565

## Bilioni 1.65 zidio la makusanyo ya ndani zatumika kuchangia miradi ya maendeleo

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri iliweza kukusanya kiasi cha Shilingi 4,905,681,185.86 sawa na asilimia 158.2 ya lengo la shilingi 3,099,407,300 na kuwa na zidio la makusanyo ya Shilingi 1,806,273,885.86 ambalo zidio hilo limeweza kuchangia miradi ya Maendeleo katika Sekta ya Afya, Elimu, Misitu, Kilimo na TEHAMA.

Kwa upande wa Shule za Sekondari,Ujenzi wa mabweni katika Shule ya Sekondari Yakobi Halmashauri ilipeleka kiasi cha Shilingi milioni 25 kuchangia nguvu za Wananchi katika Kata hiyo. “Tunatekeleza ujenzi wa mabweni matatu Block A,B na C.Mchango wa Halmashauri na nguvu za Wananchi umechangia kuweza kupata bweni moja.Kukamilika kwa mabweni haya kutatua changamoto ya ukosefu wa mabweni na pia tutakuwa na ziada ya vyumba vya kulala wanafunzi”Alisema Mkuu wa Shule Yakobi Editha John

Ujenzi wa vyumba 02 vya madarasa Shule ya Sekondari Uwemba, vyumba 04 vya madarasa na ofisi Mbeyela Sekondari na ujenzi wa vyumba 02 vya madarasa shule ya sekondari Luhololo umekamilika. Huku ukamilishaji wa vyumba 04 vya madarasa Matola Sekondari ukiwa katika hatua za mwishoni. Zaidi ya Shilingi milioni arobaini ikiwa imegawanywa kuchochea ujenzi wa majengo hayo.
“Mazingira ya kujifunzia yamekuwa bora zaidi.Wapo Waalimu wa kutosha vyumba vya madarasa vya kutosha tunaishukuru Serikali kwani kadri siku zinavyoenda mabadiliko yanayofanyika ni mengi.”Alisema Simon Ngelela Mwanafunzi kidato cha tatu Mbeyela Sekondari.

Uboreshaji wa mazingira ya Shule unaambatana na uboreshaji wa nyumba za waalimu na miundombinu bora ya uhifadhi wa maji taka.Katika shule ya Sekondari Uliwa milioni 10 ilitumika kupata mashimo ya kisasa ya choo katika nyumba 04 za waalimu.

Kwa upande wa Kata ya Utalingolo na Ramadhan wanasema kwa sasa hawataki tena kuona watoto wao wakihangaika kutafuta elimu katika shule za mbali. Ramadhani wameanza ujenzi wa shule ya sekondari Mpeto ambapo Halmashauri imewapatia kiasi cha Shilingi milioni 20 kufanikisha ujenzi wa vyumba 04 vya madarasa na Ofisi moja. Kwa upande wa Shule ya Sekondari Utalingolo wapo katika hatua za ukamilishaji wa vyumba muhimu na kuomba usajili ili shule ya Sekondari Utalingolo iweze kuanza. Kiasi cha Shilingi milioni 80, Milioni 40 ikiwa ya ujenzi wa bweni na 40 ikiwa ya ujenzi wa madarasa 04 katika Sekondari ya Utalingolo.

“Wanafunzi walikuwa wanakwenda Maheve ni mbali sana kutoka hapa na wanatembea katika misitu. Hii hali ni hatarishi ndio maana tuliona ni vyema kujenga Shule ya Sekondari Mpeto tulianza na Shule ya Msingi sasa Tumekuja kwenye Sekondari”Alisema Mwenyekiti wa Kijiji cha Mpeto Aron Lutumo

Kwa upande wa Sekta ya Elimu Msingi uboreshaji wa miundombinu ya shule chakavu na kongwe unaendelea katika shule ya Msingi Mikongo yenye ujenzi wa vyumba 07 vya madarasa, Shule ya Msingi Msindu Kata ya Kifanya ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa, Shule ya Msingi Mtila Kata ya Matola ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa na vyoo vya watumishi, ujenzi wa vyumba 03 vya madarasa Shule ya Msingi Nazareth Kata ya Mjimwema, ambapo kila moja iliweza kupatiwa kiasi cha Shilingi milioni 20 na Shule ya Msingi Mbega Kata ya Matola Ujenzi wa madarasa 5 na Ofisi 1 Kiasi cha shilingi milioni 40 lengo ikiwa kukamilisha shughuli za ujenzi katika shule hizo na kuchochea nguvu za Wananchi.
Aidha kiasi cha Shilingi milioni 10 kilitolewa na Halmashauri kukamilisha ujenzi wa matundu 16 ya vyoo mamongolo Shule ya Msingi, Milioni 8 laki 8 Matundu 18 ya vyoo Shule ya Msingi Ikisa, Shilingi, Shilingi milioni 5 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyoo vya awali matundu 8 na matundu 22 ya Shule ya Msingi Kambarage NA Shilingi million 5 ujenzi wa vyoo na Darasa la awali Shule ya Msingi Boimanda.

Upatikanaji wa elimu bora unaendana na uwepo wa mazingira bora ya kufundishia. Halmashauri imeendelea kuweka jitihada kwa kujenga nyumba bora kwa watumishi katika sekta ya Elimu Msingi ambapo kiasi cha shilingi milioni 62 laki 5 zilitolewa na Halmashauri; Milioni 60 ikiwa ni ukamilishaji wa nyumba ya Mwalimu Peruhanda, Liwengi, na Kisilo ambapo kila shule ilipatiwa kiasi cha shilingi milioni 20 na kiasi cha shilingi milioni 2.5 kukamilisha nyumba ya mwalimu shule ya msingi Mbega. Ujenzi huu upo katika hatua za ukamilishaji na Halmashauri imefanikiwa kupeleka kiasi cha Shilingi Milioni 20 ili kukamilisha ujenzi wa jengo



*Ujenzi wa nyumba ya nyumba ya Mwalimu yenye uwezo wa kubeba familia mbili "Two in One"ukiwa katika hatua za upigaji rangi Shule ya Sekondari Luhololo. Ujenzi uliotekelezwa kwa mapato ya ndani na nguvu za Wananchi*

Ukamilishaji wa Zahanati unakwenda sambamba na ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya kwenye zahanati hizo. Jambo ambalo litasaidia kupunguza uhaba wa nyumba za watumishi na kuvutia watumishi kufanya kazi katika maeneo ya Vijijini. Milioni 32 zimetolewa kuendeleza ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya katika Zahanati ya Iduchu, Igola, Itulike na Mfereke.

Ukamilishaji wa Zahanati unakwenda sambamba na ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya kwenye zahanati hizo. Jambo ambalo litasaidia kupunguza uhaba wa nyumba za watumishi na kuvutia watumishi kufanya kazi katika maeneo ya Vijijini. Milioni 32 zimetolewa kuendeleza ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya katika Zahanati ya Iduchu, Igola, Itulike na Mfereke.

Halmashauri inaendelea na utekelezaji wa sera ya afya ya mwaka 2010 inayotaka uwepo wa Zahanati katika kila Kijiji na Mtaa na kituo cha Afya kwenye kila Kata na ndio maana shughuli za Ujenzi zimeendelea kushika kasi. Kwa sasa Halmashauri na Wananchi wanaendelea na ujenzi wa zahanati ya Mamong'olo, Matola, Idihani, Makanjaula, Magoda, Kihesa, Luponde na Uliwa na hizi zote zipo katika hatua za mwisho za ujenzi. Punde si punde Zahanati hizi zitaanza kutoa huduma na kutatua changamoto ya ukosefu wa huduma za afya kwa Wananchi . Halmashauri imechangia shilingi milioni 120 kufanikisha ujenzi wa zahanati hizo.

Katika Kata ya Ihanga Kijiji cha Lwangu Halmashauri imetoa maeneo na kuanzisha vitalu vya chai (Block farm) kwa ajili ya wakulima wa chai. Aidha, kiasi cha Shilingi milioni 10 kilitolewa kwa ajili ya skimu ya umwagiliaji. Katika Kijiji cha Lilombwi Kata ya Kifanya takribani Kilomita 12 kutoka makao makuu ya Kijiji wanapatikana wakulima wa Chai wenyewe wanajiita "MTANGA BLOCK FARM"Halmashauri nayo imeweza kuwafikia kwa kuwapatia kiasi cha Shilingi milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa vibanda vya kuhifadhia chai.



*Mojawapo ya kibanda cha kuhifadhia chai kwa wakulima wa chai MTANGA katika Kata ya Kifanya ambapo Halmashauri imechangia milioni ishirini kufanikisha ujenzi wa vibanda vinne vya kuhifadhia chai*

Manufaa ya utekelezaji wa miradi hii inatokana na jitihada ambazo wananchi wameonesha katika kuibua miradi. Ukishikwa Shikamanaa ukitaka kujikuna anza na pale unapoweza kunakosalia achia wengine wakusaidie. Hivyo ndivyo Halmashauri inavyotekeleza miradi yake Wananchi wanaanza linapokuwa boma Basi Halmashauri inaweka fedha kupata mradi kamili. Afisa Mipango wa Halmashauri Shigela Ganja anaelezea utaratibu unaotumika katika kutoa fedha za kukamilisha maboma.

"Tunaongozwa na miongozo ya Serikali katika kupeleka fedha.Mwongozo uliopo sasa ni fursa na vikwazo kwa maana kuwa fedha zinazokwenda kwenye miradi zinatakiwa zikaongeze jitihada za Wanachi kwa miradi waliyoianzisha wenyewe."Alisema Ganja

Iluminatha Mwenda ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe yeye atatuelezea siri kuu ya mafanikio katika Halmashauri na mipango iliyojiwekea ya kuhakikisha maboma yote yaliyoanzishwa yanakamilika kwa wakati.
"Mwaka jana tulikuwa na fedha nyingi sana.Tulikusanya mpaka tukawa na zidio la bajeti  na ndio maana tuliweza kupeleka fedha za miradi katika vijiji na mitaa yote. Ule moyo tuliokuwa nao wa kufanya kazi kwa ushirikianao tuuendeleze.Wananchi wetu wanajitolea sana hivyo ushirikiano ndio siri ya mafanikio yote haya.Kwa sasa tunamiradi mikubwa ya vituo vya afya Kifanya na Makowo na tunaimani tutakamilisha majengo yote kama Serikali inavyoelekeza." Alisema Mwenda
.



Upendo Shari Mmoja wa wafugaji bora Kimkoa na Kikanda katika maonesho ya nanenane kwa mwaka 2020 ambapo wataalamu wa Halmashauri wamewezesha kufanikisha utoaji wa elimu bora



Wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Mbeyela wakifurahia mazingira bora ya kujifunzia ambapo Halmashauri kwa kushirikiana na Wananchi wameweza kushiriki kuibua miradi ya ujenzi wa madarasa ambayo kwa sasa yameanza kutumika

## Matukio katika Picha



*Mwonekano wa Zahanati ya Makanjaula ambapo Halmashauri na Wananchi wanaendelea na ujenzi wa zahanati ya Mamong'olo, Matola, Idihani, Makanjaula, Magoda, Kihesa, Luponde na Uliwa na hizi zote zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Halmashauri imechangia shilingi milioni 120 kufanikisha ujenzi wa zahanati*




*Picha ya pamoja ya Washiriki wa warsha ya maandalizi ya mipango ya bajeti ya afua za Lishe kwa mwaka 2020/2021 katika Halmashauri ya Mji Njombe ambapo Mkurugenzi wa TEHAMA TAMISEMI Erick Kitali alikuwa ndiye Mgeni Rasmi*